ICUD 2024 PRIZE:

S/N	AINA YA TUZO ITAKAYOTOLEWA	VIGEZO	VIELELEZO
1.	***Uwezeshaji wa huduma za Kifedha kwa makundi ya watu wenye Mahitaji maalumu (Persons with Disabilities)***	Je chama kina watu wangapi wenye mahitaji maalum?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je chama kinawahudumia watu wangapi wenye mahitaji maalum hadi kufikia mwishoni mwa Mwaka 2023?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je chama kina program yoyote inayolenga kuwajengea uwezo watu wenye mahtaji Maalum kuhusiana na huduma za kifedha zinazotolewa na chama?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je aina gani ya huduma zinazotolewa kwa wanachama hao.	Taja
		Je ni kiasi gani cha riba kinatozwa kwenye huduma hizo na zinatofautianaje na gharama nyingine zinazotozwa kwenye huduma za wanachama wengine	Taja na weka ushahidi
		Kiwango cha Mikopo kilichotolewa kwa watu wenye mahitaji maalum hadi kufikia mwaka 2023	Taja na weka ushahidi
		Je wapo watu wenye mahitaji maalum ambao wanashiriki kwenye nafasi za uongozi Chamani (Bodi na Kamati)?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je kuna sera yoyote iliyoandaliwa na chama juu ya namna ya kuhamasisha, kuvutia na kusaidia watu wenye mahitaji maalum kujiunga na kupata huduma za kifedha chamani?	Toa Maelezo na Ushahidi
		SACCOS imeandaa na kuendesha semina za mafunzo ngapi zinazohusiana na masuala ya watu wenye mahitaji maalum katika chama au eneo lako?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je chama kinao utaratibu wa kutembelea na kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum ambao si wanachama?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je chama kimewasaidia watu wangapi wenye mahitaji maalum ambao si wanachama?	Taja
		Je chama kimetoa msaada gani kwa watu wenye mahitaji maalum chamani na nje ya wanachama?	Toa Maelezo na Ushahidi

		Misaada iliyotolewa kwa watu wenye mahitaji maalum ina thamani ya Shilingi ngapi hadi kufikia Mwaka 2023?	Toa Maelezo na Ushahidi
		Je chama kinao utaratibu wa kupendelea, kurahisisha na kutoa huduma kwa watu wenye mahitaji maalumu?	Toa Maelezo na Ushahidi
2.	**SACCOS bora inayomlinda Mlaji (Consumer Protection)**	Je SACCOS yenu ina malalamiko mangapi?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Malalamiko mangapi yametatuliwa ngazi ya Chama?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Malalamiko mangapi yametatuliwa ngazi ya Mrajis?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Malalamiko mangapi yametatuliwa ngazi ya Mahakama?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je, chama kina mwongozo wa ulinzi wa Mlaji?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je, malalamiko ya wanachama huwasilishwa kwa njia gani?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je, chama kina mfumo wa kupata maoni ya namna huduma zinvyotolewa chamani?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Wanachama wangapi hawakuridhishwa na huduma zitolewazo na chama	Toa Maelezo
		Je, chama kimeandaa na kuendesha semina na mafunzo mangapi yanayohusu ulinzi wa mlaji?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je chama kinao utaratibu / program za kusaida ubunifu (Creative and Innovation) unaowezesha kurahisisha utoaji wa huduma kwa wanachama na shughuli za chama kufanyika kwa ufanisi?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Ni maazimio mangapi yaliyojitokeza kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka 2022 yametekelezwa kikamilifu kufikia 2023?	Toa Maelezo na Ushahidi
3		Je SACCOS yako imeongeza wanachama wangapi kwa kipindi cha miaka mitatu (2021, 2022, 2023)?	Toa Maelezo na Uthibitisho

	SACCOS bora inayokuwa kwa kasi (Fast Growing SACCOS) kwa daraja A na B.	Je SACCOS yako imekuza mali zake kwa kiasi gani kwa kipindi cha miaka mitatu (2021, 2022, 2023)?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je SACCOS yako imekuza Hisa, Amana na Akiba zake kwa kiasi gani kwa kipindi cha miaka mitatu (2021, 2022, 2023)?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je SACCOS yako imekuwa ikipata Hoja gani kutoka kwa Mkaguzi wa nje kwa kipindi cha miaka mitatu (2021. 2022 na 2023)?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		Je SACCOS yako imekuwa ikitekeleza Mpango Kazi wa kila mwaka kwa ukamilifu kwa kiasi gani kwa kipindi cha miaka mitatu (2021, 2022, 2023)?	Toa Maelezo na Uthibitisho
		SACCOS yako imefanya mabadiliko gani madogo, ya kati au makubwa yanayo akisi ukuaji wake?	Toa Maelezo na Uthibitisho
4.	***SACCOS bora ya jumla (Overall) inayogusa maisha na kutoa tabasamu kwa Jamii kwa kuzingatia msingi wa Ushirika wa kujali Jamii.***	Je, SACCOS yenu ina mikakati (malengo) gani katika kuijali Jamii kwa kuzingatia msingi wa Ushirika wa kuijali Jamii?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, ni kwa kiasi gani SACCOS yenu imefikia malengo mliyojiwekea katikashughuli za kuijali Jamii?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, kwa mwaka 2023 ni shughuli gani ambazo SACCOS yenu imefanya katika kuijali Jamii.	Toa maelezo
		Je, kwa mwaka 2023 SACCOS yako ilitumia kiasi gani cha fedha katika kutekeleza shughuli za kuijali Jamii?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, kwa mwaka 2023 SACCOS yako imewafikia wahitaji wangapi?	Toa maelezo na uthibitisho
		Tafadhali eleza athari za shughuli/misaada iliyotolewa na SACCOS yenu kwa jamii mlizozifikia.	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, SACCOS yenu inashirikiana na Vyama vingine vya Ushirika kwa ajili ya kufanikisha msingi wa kuijali Jamii?	Toa maelezo na uthibitisho
		Ni changamoto gani kubwa ambazo SACCOS yenu imekumbana nazo katika kutekeleza shughuli za kuijali jamii?	Toa maelezo

		Tafadhali eleza jinsi mlivyokabiliana na changamoto hizo na suluhisho mlilopendekeza.	Toa maelezo na uthibitisho
5.	***SACCOS Bora Inayochochea Huduma Jumuishi Za Kifedha Vijijini***	SACCOS inapatikana eneo gani? Mkoa, Wilaya, Mtaa nk	Toa maelezo na uthibitisho
		SACCOS yako inatoa huduma zake kwa gharama gani? (Riba/Ada n.k)	Toa maelezo na uthibitisho
		SACCOS yako ina matawi au vituo vya huduma? Na vipo kwenye maeneo gani?	Toa maelezo na uthibitisho
		Ni aina gani za bidhaa na huduma za kifedha ambazo SACCOS hutoa?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je SACCOS yako ina bidhaa/huduma au programu maalumu kwa maeneo ya vijijini?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je SACCOS yako inatoa mafunzo ya elimu ya fedha kwa wanachama wa vijijini?	Toa maelezo na uthibitisho
		SACCOS inahakikisha vipi huduma zake zinawafikia watu wa vijijini na wale ambao hawajapata huduma, hasa wanawake, vijana na makundi maalum?	Toa maelezo na uthibitisho
		SACCOS inatumia mfumo wa kidijitali kwenye kufikisha huduma kwa wanachama walio mbali?	Toa maelezo na uthibitisho
		Ubunifu gani umewekwa ili kushughulikia changamoto za jamii za vijijini, kama vile umbali au viwango vya chini vya kujua kusoma na kuandika ili kushiriki kwenye huduma zinazotolewa na SACCOS?	Toa maelezo na uthibitisho

6.	***Chama Cha Kijamii Kinachoshirikisha Wanachama Wake Kikamilifu (Member Engangement)***	Je, wanachama wanahusika vipi katika mchakato wa kufanya maamuzi?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, wanachama wanashirikishwa katika maamuzi kwenye mikutano mikuu inayofanyika kuanzia ngazi ya chini?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, kuna mpango mahususi wa kuwafikia wanachama kimasoko/elimu au uwasilishaji wa taarifa?	Toa maelezo na uthibitisho
		Ni taarifa za aina gani ambazo wanachama wanazipata nje ya utaratibu wa Mikutano Mikuu?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, SACCOS yako inafanya tathmini ya mahitaji ya mara kwa mara au tafiti?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, wanachama wanafahamu kuhusu Dira, Dhima ya Chama pamoja na Mipango ya Chama?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, wanachama wanafahamu vema kuhusu Chapa (Brand) na huduma/bidhaa za SACCOS yako?	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, Chama chako kinatumia mbinu za kidijitali kuwasiliana au kukutana na wanachama *(Tovuti, mitandao ya Kijamii etc)*	Toa maelezo na uthibitisho
		Je, Chama chako kinatumia mfumo/utaratibu gani kwenye kupima kuridhika kwa mwanachama?	Toa maelezo na uthibitisho

1. **VIGEZO VYA KUSHIRIKI:**

i. Mshiriki lazima awe ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kilichosajiliwa kwa mujibu wa taratibu na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2023 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2015. Aidha, SACCOS hizo zinapaswa kuwa zinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2019.
ii. Ni lazima kutaja JINA LA CHAMA, NAMBA YA USAJILI, NAMBA YA LESENI, MKOA na WILAYA kinapopatikana pamoja na namba ya Simu ya Meneja.
iii. Mbali na utoaji huduma za kawaida, Chama lazima kiwe kinajishughulisha na utoaji huduma kwenye kipengele husika cha tuzo.
iv. Chama kishiriki kinapaswa kutoa Ushahidi na uzoefu wa huduma husika kwenye kipengele cha Tuzo anachoshiriki.
v. Taarifa zitakazowasilishwa zinapaswa kuwa za kweli na zilizothibitishwa na uongozi na Menejimenti ya chama husika. Kutoa taarifa za uongo ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria, hivyo chama husika kinaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa ukiukwaji huo pale itakapobainika.

2. **TARATIBU ZA KUWASILISHA MAOMBI/TAARIFA:**

i. Chama kinaweza kushiriki kwenye tuzo zaidi ya moja kutegemeana na sifa na vigezo vilivyopo kwenye tuzo hiyo.
ii. Fomu/Taarifa zote zinapaswa kujazwa kikamilifu kwa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye JEDWALI na kuwasilisha VIELELEZO pale inapobidi.
iii. Vielelezo vyote vya udhibitisho vinapaswa kuwa kwenye mfumo wa PDF
iv. Fomu iliyojazwa kikamilifu pamoja na vielelezo vyake, vinapaswa kuwasilishwa kwa barua pepe: prize.icud@sccult.tz
v. Mwisho wa kuwasilisha fomu/taarifa za ushiriki ni tarehe 04 Oktoba, 2024, Saa tisa na nusu alasiri (9:30 Alasiri)
vi. Kwa maelekezo zaidi wasiliana na: CPA (T) Gift Ndosi 0716 285 282 (Mratibu) .